East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 8, Issue 1, 2025
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Tathmini ya Athari ya Utabaka na Ukengeushi Katika Tamthilia ya Kigogo

*Mercy Muthoni Kariuki[1*], Prof. James Onyango Ogola, PhD[1] na Prof. Nabea Wendo, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L. P. 1100-20300 Nyahururu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: Mercykariuki135@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*28 Januari 2025*

**Istilahi Muhimu**:

*Utabaka, Ukengeushi na Tamthilia*

**IKISIRI**

Utabaka ni hali ya kuwagawanya watu kwa misingi ya uwezo wao wa kumiliki wa mali ilhali ukengeushi ni hali ya kumfanya mtu afuate njia ambayo si nzuri kwa kumlaghai. Hali hii husababisha migogoro miongoni mwa wahusika. Tamthilia ni kipengele cha fasihi andishi kinachowasilisha ujumbe kwa kutumia mazungumzo baina ya wahusika. Tafiti za awali katika tamthilia zilishughulikia matumizi ya lugha, mandhari, na uhusika katika tamthilia. Katika kupitia tafiti na makala mengine ya awali, mwandishi hajakumbana na tafiti kuhusu masuala ya utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya Kigogo. Hili ndilo pengo la kiusomi ambalo lilichochea utafiti huu kufanywa ili kulijaza. Makala yalinuia kutathmini athari za utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya Kigogo iliyoandikwa na Pauline Key. Matini yalichanganuliwa kwa kutumia misingi ya nadharia ya umarx iliyoasisiwa na Karl Heinrich Marx na kuendelezwa na wataalam kama Karl Kautsky, George Plekhanov na György Lukács. Utafiti ulifanywa maktabani ambapo athari za utabaka na ukengeushi kutokana na usomaji wa kina yalidondolewa kwa minajili ya uchanganuzi na uwasilishaji kwa kutumia mihimili ya nadharia ya umarks. Tamthilia hii ilichaguliwa kimaksudi kwa sababu inaangazia athari za utabaka na ukengeushi ambayo ndiyo mada ya makala haya. Mbinu ya kimaelezo ilitumiwa katika kuwasilisha na kuchanganua data. Usomaji wa kina wa tamthilia hii ulibainisha kuwa utabaka na ukengeushi husababisha ufisadi, ukosefu wa kazi, uchafuzi wa mazingira, ukosefu wa maendeleo, mapendeleo, kufungwa kwa soko, mauji, usherati, unyakuzi wa mashamba, chuki, uvamizi na ukombozi. Makala haya yana mchango katika uchambuzi wa vitabu teule vya fasihi andishi katika kueleza maudhui ya utabaka na ukengeushi. Utafiti huu pia ulitumiwa kama mwongozo kwa wasomi wengine watakaofanya utafiti katika fasihi andishi.

**APA CITATION**

Kariuki, M. M., Ogola, J. O. & Wendo, N. (2025). Tathmini ya Athari ya Utabaka na Ukengeushi Katika Tamthilia ya Kigogo. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(1), 105-116. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

**CHICAGO CITATION**

Kariuki, Mercy Muthoni, James Onyango Ogola and Nabea Wendo. 2025. "Tathmini ya Athari ya Utabaka na Ukengeushi Katika Tamthilia ya Kigogo". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (1), 105-116. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

**HARVARD CITATION**

Kariuki, M. M., Ogola, J. O. & Wendo, N. (2025) "Tathmini ya Athari ya Utabaka na Ukengeushi Katika Tamthilia ya Kigogo", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), pp. 105-116. doi: 10.37284/jammk.8.1.2645

**IEEE CITATION**

M. M., Kariuki, J. O., Ogola & N., Wendo "Tathmini ya Athari ya Utabaka na Ukengeushi Katika Tamthilia ya Kigogo", *EAJSS*, vol. 8, no. 1, pp. 105-116, Jan. 2025.

**MLA CITATION**

Kariuki, Mercy Muthoni, James Onyango Ogola & Nabea Wendo. "Tathmini ya Athari ya Utabaka na Ukengeushi Katika Tamthilia ya Kigogo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 1, Jan. 2025, pp. 105-116, doi:10.37284/jammk.8.1.2645.

## UTANGULIZI

Waandishi wa fasihi huangazia masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Masuala haya huwekwa pamoja na kuunda maudhui katika kazi husika. Kulingana na Kinoti, (2019) wahusika ni viumbe muhimu sana katika uendelezaji wa dhamira na katika kazi ya fasihi. Maudhui haya hunuia kuiburudisha, kuionya na kuingoza jamii. Maudhui haya huweza kuwa uongozi, ufisadi wa viongozi, ndoa, utabaka na ukengeushaji wa viongozi. Wakishughulikia tamthilia teule nchini Kenya, Wanyonyi na Nyandiba (2016), waligundua kuwa tamthilia ambazo zimetahiniwa kwa wanafunzi wa kidato cha nne nchi Kenya tangu 1998 – 2016 ziliangazia maudhui hasi. Baadhi ya maudhui yaliyoshughulikiwa ni ukabila, utabaka, ufisadi, vita, uchoyo, uchochezi, unyanyasaji, ubaguzi, ubinafsi, dhuluma, chuki, ubabedume na usaliti. Uhasi wa maudhui unaonyesha uozo katika uongozi katika nchi ambazo tamthilia hizo zimeandikwa.

Ukengeushi ni mabadiliko ambayo wahusika hupitia wakati wanapoingia katika mazingira mapya. Mabadiliko haya hutokea ili kukabiliana na chanagamoto zinazowakumba katika ugeni wa mazingira husika. Wahusika hubadilika wakiingia katika mazingira mapya kwa sababu ya ubaguzi unaotokea katika mazingira haya mapya. Mayieka, (2015) anadai kuwa ukengeushi unaotokea mara nyingi ni ule wa kitabia na ukengeushi wa kijamii. Anaendelea kueleza kuwa mabadiliko katika tabia za wahusika hutokea kwa sababu mbili. Kwanza ni kwa sababu ya malezi wakiwa wadogo na pili ni msukumo unaotoka kwa jamii. Wahusika hukengeuka ili wakubalike katika maisha na mienendo ya kisasa. Kwa hivyo ukengeushi ni hali ya kukiuka kanuni fulani na jinsi mambo huendelezwa (Tendwa, 2017).

Utabaka na ukengeushi umesababisha umasikini katika nchini zinazoendelea. Hali hii imesababishwa na unyonyaji wa mataifa yaliyoendelea kwa nchi zinazoendelea (Omoga, 2018). Hali hii inadhihirisha kuwa utabaka na ukengeushi ni masuala ambayo hutokeo kote ulimwenguni. Wakati wa wakoloni, hali ya utabaka na ukengeushi ndipo wakoloni waliwanyanyasa Waafrika katika nchi zilizotawaliwa na wakoloni. Utabaka huu ulidhihirika kupita njia mbalimbali kama vile ubaguzi wa rangi, hali za kiuchumi na kisiasa za kimapendeleo. Wakoloni walitumia mbinu hii ili kuchukua mali ya Waafrika ambao walionekana kuwa wa tabaka la chini kwa manufaa yao wenyewe na nchini zao. Fasihi kama kio cha jamii, masuala ya utabaka na ukengeushi yamewasiliswa katika tamthilia ya Kiswahili kama vile tamthilia ya *Kigogo* iliyoandikwa na Pauline Kea. Utabaka na ukengeushi una athari mbaya kwa wanajamii kama ilivyowasiliswa katika makala hii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

### Tamthilia ya Kigogo

Tamthilia ya Kigogo inahusu mhusika kwa jina Majoka ambaye ni kiongozi wa Sagamoyo. Majoka anatumia vibaraka wake kama vile Kenga kuwanyanyasa wananchi. Mazingira katika soko la Chapakazi ni chafu kwa sababu usafi haufanywi lakini wafanyibiashara kama vile Ashua wanatoshwa ushuru pamoja na kitu kidogo juu yake. Majoka anatumia pesa za umma kwa njia mbaya kwa kufadhili miradi isiyokuwa na manufaa kwa wananchi kama vile kulipa yule atakayechonga kinyago cha Majoka. Majoka anampa kibali Mamapima cha kuuza pombe haramu kwa wananchi. Tunu anapigania uongozi lakini wananchi walio walevi hawampendi kwa sababu yeye ni mwanamke. Mwisho wananchi wanaungana na kumtoa Majoka mamlakani na kumchagua Tunu kuwa kiongozi wao.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Wataalam mbalimbali wamelishughulikia suala la athari ya utabaka na ukengeushi kwa namna tofautitofauti. Kwa mfano, Ndemo (2014) alihakiki nyimbo za umoja na maridhiano nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 na 2008 na kubainisha kuwa watu wengi walifariki kwa sababu ya kupigania uongozi. Anaeleza kuwa viongozi waliwakengeusha wafuasi wao wazue vita ili wao wabaki uongozi ambao ungewaweka katika tabaka la juu huku wafuasi wao wakibaki katika tabaka la chini. Masinde (2016) anadai kuwa vita kati ya familia tajiri na zile masikini imesababisha chuki katika ya familia hizi katika tamthilia ya *Buriani*. Kulingana na Masinde (2016), hivi ni vita vya kitabaka ambapo tabaka la chini linaona linanyanyaswa na tabaka la juu. Haji (2018) anasema kuwa migogoro kati ya tabaka la juu na lile la chini husababisha hali ya umasikini kwa sababu wananchi hutumia muda wao kupigania raslimali chache zilizo chini badala ya kujishughulisha na masuala ya kimaendeleo. Mwaniki (2018) alibainisha kuwa watu walio mamlakani katika diwani ya *Bara Jingine*, shairi la *Wanabiashara Barabarani*, wanatumia njia za mkato ili kujipatia mali ilhali watu masikini wakiteseka. Kwa hivyo viongozi wanatumia vyeo vyao kujipatia mali ambayo inastahili kutumiwa na kila mwananchi.

Utabaka katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* unasababisha chuki baina ya wahusika wa Kiafrika na wale wa Ugenini (Musyoki, 2016). Chuki hii inajitokeza kwa sababu tabaka la juu linawanyanyasa wanachi wa tabaka la chini. Tabaka la juu linajiona kuwa bora zaidi kuliko lile la chini. Abdille na wenzake (2017) wanasema kuwa utabaka umesababisha umasikini katika riwaya ya *Walenisi*. Wanaeleza kuwa mwandishi amemtumia mhusika Dzombo kuonesha dhamira ya umasikini katika riwaya hii. Mhusika anaonekana akiishi katika dimbwi la ufukara. Gakii (2019) alibainisha kuwa ukombozi katika tamthilia ya Kifo kisimani na *Fumo Liyongo* ulipatika baada ya baadhi ya wananchi kujitolea mhanga ili kupigania haki zao. Wananchi waliokuwa wamechoka na kunyanyaswa na matajiri walijitokeza ili kupigania usawa katika nchi zao.

### Nadharia ya Umarks

Uchanganuzi na uwasilishaji wa data katika makala hii ulitumia nadharia ya umarks. Kulingana na Mhando (2015), nadharia ya umarks iliasisiwa na Karl Marx katika karne ya kumi na tisa katika bara la Ulaya na baadaye nadharia hii ikasambaa kote duniani. Nadharia hii ilizuka kwa sababu ya kukosoa serikali za kipebari ambazo zilisheheni unyonyaji na ukandamizaji wa wananchi masikini. Nadharia hii inasisitiza kuwa kuna mgongana wa kimatabaka katika Maisha. Kuna tabaka la chini la wasionacha na tabaka la juu la walionacho. Wananchi wa tabaka la juu huwanyanyasa wale wa tabaka la chini kwa kuwafanyiza kazi nyingi kwa muda mrefu ili kujiongezea faida. Masikini hupigania haki zao kwa kutumia migomo, hali inayosababisha migogoro ya kijamii.

Kulingana na Castle (2007), fasihi ni msukumo wa jamii na mitazamo yake. Hii ndio maana hata fasihi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

huonyesha matabaka yanayopatikana katika jamii. Kazi za kimarx huonyesha mikinzano ya kitabaka na uhusiano kati ya fasihi na muundo wa kiuchumi katika jamii hudhihirika. Maendeleo ya historia ya binadamu pamoja na taasisi zake ni zao la mabadiliko katika njia za kimsingi za uzalishaji mali. Kwamba mabadiliko kama hayo husababisha mageuzi katika muundo wa matabaka ya kijamii ambayo katika kila kipindi huendeleza kung'anga'aniwa kwa uwezo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii; na kwamba dini, fikra na utamaduni wa jumuia yoyote ni itikadi na miundo maalum ya kitabaka inayozaa miundo na matabaka ya kijamii.

Kwa mujibu wa Mwenda (2004), matabaka huzalisha mkururo wa miundo ya urazini inayoshindana na kukinzana. Kazi za kimarx huhusisha itikadi na uzalishaji mali na jinsi inavyoathiri mivutana ya kisiasa. Waandishi wa kimarx humithilisha kazi zao na hali halisi katika maisha ya binadamu wakati kazi hizo zilitungwa. Kazi kama hizi huonyesha maudhui na jinsi ya kuyaboresha maisha. Fasihi kulingana na umarx hueleweka tu katika hali halisi ya binadamu. Nadharia hii hukumbwa na changamoto ya kuweza kuchagua kiwango cha maisha kitakachozingatiwa. Ni vigumu kuzingatia maisha kwa ujumla wake.

Kulingana na haya, nadharia ya umarks ina mihimili ifuatayo;

- Watu kutangamana.
- Viongozi huwasimamia watu na mali kisha kuwafanya watawaliwa.
- Kuna unyanyasaji unaoletwa na viongozi.
- Kuna hamasisho kwa wanajamii.
- Kuna vizuizi katika kuafikia malengo.
- Kuzinduka kwa wanajamii dhidi ya vizuizi.
- Mapinduzi yanayosababisha vifo na kuleta mwanzo mpya.

Makala haya yalitumia mhimili wa saba unaosema kuwa katika jamii ya matabaka huwa na mapinduzi yanayosababisha vifo na kuleta mwanzo mpya. Mhimili huu ulitumiwa kutathmini athari za utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya *Kigogo*.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo kwa sababu data za utafiti huu zilikuwa za kithamano. Utafiti huu ulifanywa maktabani ambapo mtafiti alisoma tamthilia ya *Kigogo* (2016) iliyoandikwa na Pauline Keya. Tamthilia hii ilichaguliwa kimaksudi kwa sababu inaangazia masuala ya utabaka na ukengeushi kwa mapana. Mbinu ya kimaelezo ilitumiwa katika uwasilishaji wa data katika utafiti huu baada ya hoja zote zinazoangazia athari za utabaka na ukengeushi kudondolewa na mifano kutolewa kama idhibati.

## MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo ya utafiti huu yalitokana na usomaji wa kina wa kina wa tamthilia ya Kigogo iliyoandikwa na Pauline Keya. Hoja zilizoangazia athari ya utabaka katika tamthilia hii zilidondolewa kwa minajili ya uchanganuzi na uwasilishaji. Uwasilishaji na uchannganuzi huu ulitumia misingi ya nadharia ya umarks. Mhimili wa nadharia ya umarks unaodai kuwa kuna mapinduzi yanayosababisha vifo na kuleta mwanzo mpya ulitumiwa kutathmini athari za utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya Kigogo. Yafuatayo ndiyo matokeo ya utafiti huu.

### Ufisadi

Ufisadi hutokea wakati viongozi wanatumia mali ya umma kujinufaisha wao wenyewe na watu wengine walio karibu nao. Katika nchi ya Sagamoyo katika tamthilia ya *Kigogo*, wanyanyibiasha kama vile Ashua, Kombe na Boza wanatoa hongo kwa watawala wao kama vile Majoka. Pia kando na kodi wanayotoza wafanyibiashara kila mwezi, wafanyibiashara hawa hutoa kitu kidogo kwa wenye nchi. Wale ambayo hawana hiari ya kutoa kitu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

kidogo wananyanganywa kila kitu walicho nacho. Hali hii inajidhihirisha katika dondoo lifuatalo.

> *Kombe: (Akiinua kichwa na kumtazama Ashua) Ndio hali ya maisha bibiye. Wajua lazima tutie tonge kinywani na tuwape wenye nchi kitu kidogo. Biashara iko vipi kwenye vioski vyenu?*

> *Ashua: tunajaribu tu japo hakukaliki huko. Uvondo na kuhangaishwa na wenye nguvu ndiyo hewa tunayoipumua huko. Kwetu wanadai kitu kikubwa au kitu chote. (UK 2)*

Dondoo hili linaonyesha jinsi matajiri ambao ni wenye nchi wanatumia mamlaka kuchukua mali ya watu masikini kwa njia ya kodi. Wenye nchi ambao ni viongozi matajiri wanawahangaisha wanabiashara kwa nia ya kuwanyang'anya kidogo ambacho wameuza.

Kwa upande mwingine, Boza amekengeushwa. Boza haoni shida ya serikali kukusanya kodi kutoka kwa wananchi. Kwake ni sawa serikali ikinyanyasa wafanyibiashara wadogo. Kwa hio ni kawaida. Boza hajatambua kuwa kodi wanayolipa si kodi tu bali ni kodi na kitu juu yake ambacho sasa si halali. Haya yanajidhihisha katika dondoo lifuatalo,

> *Boza: (Akimkazia Kombe macho.) Acha kulalamika! Ni jukumu lao kukusanya kodi nawe ni sharti ulipe kodi hiyo bwana. Huko ni kujenga nchi na kujitegemea. (UK 2)*

**Uchafuzi wa Mazingira**

Mazingira machafu husababisha magonjwa kwa wananchi na viumbe wengine. Mazingira ya soko la chapakazi ni chafu. Karibu na karakana ya akina Boza, Kombe na Sudi kuna mtaro ambao unapitisha maji machafu na tena yananuka. Mazingira haya ni machafu ndio maana kuna harufu mbaya inayowasumbua fundi wanapofanya kazi yao. Viongozi pia wanakusanya kodi lakini hawataki kuhakikisha kuwa soko ni safi. Wanakusanya tu kodi na soko halisafishwa. Ndio maana Sudi analalamika hivi,

> *Sudi: Ni jukumu lao pia kuhakikisha soko ni safi, si kukusanya kodi pekee … na si haki kuchukua kilicho chetu na kututishatisha….(UK 3)*

Wafanyibiashara wanalipishwa kodi lakini haieleweki ni wapi pesa zinapelekwa kwa sababu pesa za kusafisha soko zinatolewa na wafanyibiashara lakini wao wanaendelea kukaa katika mazingira machafu.

**Ukosefu wa Maendeleo**

Maendeleo ni hali ya kuboresha miundo msingi ya taifa ili kuboresha Maisha ya wananchi. Haji (2018) anasema kuwa nchi zenye utabaka hupoteza muda mwingi katika mapigano na kusahau masuala ya maendeleo. Nchi ya Sagamoyo licha ya kuwa na miaka sitini kabla ya kupata uhuru, hakuna maendeleo ambayo wananchi wanaweza kujivunia. Maendeleo ambayo yamefanyika ni machache sana. Hotuba ya kiongozi wa nchi ya Sagamoyo, Majoka, wananchi wanaarifiwa kujivunia kuwa na kampuni kubwa ya uzalishaji wa sumu ya nyoka barani. Licha ya kutokuwa na maendeleo ya kuwasaidia wananchi, kiongozi wa nchi Bwana Majoka anatangaza mwezi mzima wa kusherehekea siku ya kuadhimisha uhuru. Katika mwezi huu, wananchi watapumzika na hawana chakula nyumbani mwao. Katika hali hii Boza bado amekengeuka na haoni kuwa mwezi mzima wa kusherehekea ni makosa kwa sababu wananchi hawatakuwa na chakula. Yeye anamlaumu Sudi kuwa anaweka siasa kwa kila kitu.

> *Boza: Wewe nawe hukualikwa. Wataka kutia siasa tayari? Hamkosi kutia doa kila jambo zuri ? (UK 5)*

Boza anamalaumu Sudi kwa kuikosoa serikali ya Majoka kwa kutoa mwezi mzima wa mapumziko kwa ajili ya kusherehekea siku ya uhuru. Kwake si shida wakiwa na mwezi mzima wa mapumziko. Hii ni kwa sababu Boza amekengeuka na haoni shida na serikali ya Majoka.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

**Mapendeleo**

Mapendeleo hutokea ikiwa kuna wananchi wanapewa huduma bora kuliko wengine. Ni hali ambapo wananchi hawapewi huduma sawa. Kuna mapendeleo katika serikali ya Majoka. Mapendeleo yanatokea katika kupeana kandarasi ya kuoka keki ya siku ya kuadhimisha uhuru wa nchi. Kandarasi hio alipewa Asiya kwa sababu ya uhusiano wake wa karibu na mkewe Majoka, Husda. Kwa hivyo familia ya Boza inastahili kuwa na furaha kwa sababu Asiya ndio mwokaji wa Keki ya uhuru na si keki moja bali keki sitini. Dondoo lifuatalo linaonyesha jinsi uhusiano wa karibu kati ya Husda na Asiya ulisababisha Asiya kupewa Kandarasi ya kuoka keki ya kuadhimisha siku ya uhuru.

> *Kombe: Sasa naelewa, waokaji keki wana kazi. Mkeo aliipata ile kandarasi?*
>
> *Boza: Aikose? Asiya ni mwanamke halisi bwana! Amemweka Bi Husda hapa. (Akiashiria kwapani.) Yeye na Ngurumo walimwandama Bi. Husda hadi wakapewa kandarasi. (UK 6-7)*

Hii inamaanisha kuwa kandarasi haikupenwa kwa njia wazi. Kandarasi ya kuoka keke ya uhuru ilipeanwa kwa sababu Husda ana uhusiano mzuri na Asiya na Ngurumo.

Kenga ambaye ni mshauri mkuu wa kingozi wa nchi, Majoka alipewa kazi hio kwa sababu yeye ni binamuye wa Majoka. Katika kejeli yake, Sudi anasema wametembelwa na binamuye Majoka.

> *Sudi: (Anasita kidogo huku sauti ya mawazo yake inasikika.) Mshauri mkuu na Binamuye Majoka amelitembelea soko la walalahoi, lo! Sa sa ninaamini kuwa tunasherehekea miaka sitini ya uhuru. (UK9)*

Kuna mapendeleo katika kufunga vyombo vya habari. Majoka anaamrisha kufunga runinga ya Mzalendo na kuiwacha Runinga ya Sauti Mashujaa. Runinga ya Mzalendo inafungwa kwa sababu inawapeperushia wananchi yale yanayoendelea katika maandamano. Runinga ya Sauti ya Mashujaa inawachwa kwa sababu haiwaambii watu ukweli wa mambo yanayoendela katika maandamano.

> *Majoka: Sudi. Sudi hatanikosesha usingizi, laiti angalijua salamu zinazomsubiri hapa! Na hii runinga ya Mzalendo nayo haina maisha Sagamoyo. Kitabakia kituo kimoja tu!*
>
> *Kenga: Sauti ya Mashujaa peke yake. (UK 37)*

**Matumizi ya Ufadhili kwa Miradi ya Kibinafi**

Kila nchi hupata ufadhi kutoka nchi zingine au mashirika mbalimbali ili kuendeleza miradi muhimu katika taifa. Viongozi wanastahili kutumia ufadhili huu ili kuboresha Maisha ya wananchi. Katika nchi ya Sagamoyo, Majoka anatumia ufadhili uliotolewa na nchi za Magharibi na Mashariki kwa manufaa yake mwenyewe. Uanatumia ufadhili huo kwa mradi ambao hauna manufaa kwa wananchi. Ufadhili uliotolewa na nchi za Kimagharibi na kuwapa Kombe, Boza na Sudi mradi wa kuchonga kinyago chake mwenyewe ili kitumiwe katika siku ya kuadhimisha siku ya uhuru wa nchi ya Sagamoyo. Anatumia mradi huu ili kumshinikiza Sudi awache kumpinga kama mpinzani wake.

> *Kenga: Boza stop it! (Anatua kisha anamtazama Sudi.) Mlipo yake mazuri Sudi. Mradi huu utayabadilisha maisha yako. Jina lako litashamiri. Utapata tuzo nyingi paia. Kuna likizo ya mwezi mzima ughaibuni; na familia yako. Ninavyokujua wewe kazi hiyo kwako ni mteremko. Na ni nani ajuaye, watakapoiona kazi yako wageni wetu pengine. (Uk 11-12)*

Haya maelezo ya Kenga yanaonyesha jinsi mali ya umma inavyotumiwa kwa kazi za kibinafsi. Pesa za mkopo ambazo wanasagamoyo watalipia kwa miaka mia moja. Hii ni kuhakikisha Wanasagamoyo walio katika tabaka la chini kwa sababu ya kutozwa ushuru kwa muda mrefu. Kenga anajaribu kuwakengeusha Sudi, Boza na Kombe kwa kuwapa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

keki. Sudi ana msimamo dhabiti anaikataa keki hio kwa sababu anajua ni njia ya kuwapumbaza ili wasipinge mipango mibaya ya serikali ya Majoka. Sudi anashangaa kwa nini wao wapate keki kidogo ilhali Sagamoyo ni kwao, keki ni yao, sherehe ni yao na ufanisi pia ni wao. Anashangaa keki kubwa ni ya nani. Hivi ndivyo raslimani ya Sagamoyo inavyogawanishwa. Watu maskini wanapata kidogo sana ilihali raslimali kubwa inatumiwa na wale wa tabaka la juu.

**Kufungwa kwa Soko**

Katika jamii inayotegemea biashara ili kukimu maslahi yao, soko ni muhimu sana katika Maisha ya wanajamii hawa. Wao hutumia soko kukunua na kuuza bidhaa yao. Abdille na wenzake (2017) wanadai kuwa utabaka husababisha hali ya umasikini katika taifa. Katika nchi ya Soko la Chapakazi linafungwa na serikali ya majoka. Soko linafungwa bila kujua kuwa wananchi wa tabaka la chini kama vile Boza, Kombe, Ashua na Sudi wanapata riziki na mahitaji mengine kule. Majoka pia analifunga soko la Chapakazi ili kumpata Ashua ili afanye mapenzi naye. Alijua akifunga soko la Chapakazi, Ashua atakosa chakula na kuenda kwake kuomba ili ampate.

Sababu nyingine ya kufunga soko ilikuwa kumkengeusha Sudi achonge kinyago. Walijua vizuri Ashua akikosa chakula ataenda kwa Majoka kuomba. Kisha atatiwa ndani wakati watazua vurugu na Husda. Akitiwa ndani hatawachiliwa hadi mmewe Sudi amchongee Majoka kinyago.

> *Majoka: hatimaye huyo Ashua ameanguka mtegoni.*
>
> *Kenga: Yuko ndani?*
>
> *Majoka: Bila shaka.*
>
> *Kenga: (Akinyoshea Majoka kidole.) Kazi safi.*
>
> *Majoka: Kila kitu kiko shwari. Namtarajia Sudi wakati wowote.*
>
> *Kenga:Alijitia kiburi bandia. Hatakuwa na budi sasa kukuchongea kinyago ndipo mkewe aachiliwe. (Uk 31)*

Haya mazungumzo kati ya Kenga na Majoka yanaashiria kuwa Ashua alitiwa gerezani ili kumshinikiza Sudi ambaye ni mmewe amchongee Majoka kinyago. Kenga anasema kuwa lazima Sudi amchongee kinyago ndipo mkewe aachiliwe.

Soko linafungwa ili shamba la soko lichukuliwe na Majoka na kujenga hoteli yake ya kibinafsi. Hili ni shamba la umma ambalo linastahili kutumiwa katika shughuli za umma.

> *Tunu: (Kwa hamaki) Usinifanyie masihara! Ninakukumbusha kuwa Wanasagamoyo wana haki ya kuishi, na ugatuzi sio unayakuzi. Nasikia mmebomoa vioski kwenye soko la Chapakazi . hiyo hoteli haijengwi ng'o!*
>
> *Majoka: Nitaijenga mpende msipende. (uk 45)*

Hili ni dhihirisho kuwa soko limefungwa na vioski kubomolewa ili shamba hilo linyakuliwe na Majoka na kujenga hoteli ya kibinafsi.

**Mauaji na Maumivu**

Mauaji na maumivu hutokea kwa sababu wanajamii wanang'ng'ania raslimali za taifa. Hali hii huzua vurugu na migogoro katika maenea mbalimbali nchini. Katika maandamano katika kampuni ya Majoka and Majoka company, kuna watu ambao waliuawa na polisi. Vijana watano ambao walikuwa wakiambatana waliuawa. Kuna watu wangine ambao wameumizwa kwa sababu walikuwa wakiandamana ili soko lifunguliwe.

> *Sudi: Wameua kina nani?*
>
> *Siti: vijana watano. Wachuuzi sokoni waliokuwa wakiandamana pia wameumia … (uk 16)*

Kenga anapendekeza kuwa maandamano yatangazwe kuwa haramu na askari waamrishwe

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

kutumia nguvu zaidi. Matumizi ya nguvu za polisi inamaanisha kuwa watu wengi wataumizwa na hata wengi kufariki.

> *Kenga: Tangaza kuwa maandamano hayo ni haramu kisha uwaamuru maafisa wa polisi watumie nguvu zaidi. ( uk 34)*

Hili ni pendekezo la kuwaumiza wananchi na kuwaua wengine.

> *Kenga: Niko tayari kuwaweka mahali pao; mmoja baada ya mwingine. Huenda wamesahau lililompata jabali*
>
> *Majoka: ( Anaagua kicheko.) Ha-ha-ha-ha ... wamesahau vipi wasilolijua? Wewe Kenga ni hatari. Hata hicho chama chake cha Mwenge kilimfuata huko ahera. ( Wanagoteana konzi na kucheka kwa pamoja.)*
>
> *Kenga : Ukitaka kuwafurusha ndege, kata mti. Hawa wangekuwa wametuliza nafsi zao kwingineko. Nasikia Tunu anataka kuleta wachunguzi wa nje kuangalia upya ajali hio ya Jabali. (Uk 34- 35)*

Kenga na Majoka walipanga kifo cha Jabali ambaye alikuwa mpinzani wake katika uchaguzi uliopita. Kama mwananchi wa tabaka la juu hataki watu wengine wawe katika tabaka hilo. Wanajaribu kuwafinya chini wote ambao wanajaribu kuvuka mpaka huo. Kwa sasa Kenga na Majoka wanapanga kumuua Tunu ambaye pia anajaribu kupigania haki za wananchi wa tabaka la chini.

Majoka anaagiza vitosamachozi vitumike kuwatawanya waandamanaji. Vitosamachozi vikitumiwa, kuna wananchi ambao wataumizwa katika maandamano haya.

> *Majoka: (Kwa bezo.) Yes sir! Chopi utamwaga unga. Mbona polisi hawajawatawanya waandamanaji? Mnasubiri wafike hapa ofisini wanimalize kwanza ndipo mchukue hatua?*
>
> *Chopi: Pole Mzee.*
>
> *Majoka: Nataka kila askari akae mahali pake. Vitosamachozi viletwe vya kutosha.*
>
> *Chopi: Hata risasi. (Uk 38)*

Hii ni hatari kwa wananchi kwa sababun risasi zitawaua wananchi na vitosamachozi vitawaumiza wanannchi ambao watakuwa wakiandamana.

Tunu anamuita Majoka kuwa wao ni wauaji kwa sababu ya vijana watano ambao wameuawa katika maandamano na anamwambia Majoka kuwa atalipia kwa kila tone la damu ambayo imemwagika Sagamoyo.

> *Tunu: Mtalipa kila tone la damu mlilomwaga Sagamoyo; wewe na watu wako. (Uk 43)*
>
> Dondoo hili linaonyesha kuwa kuna watu ambao Majoka ameua. Tunu anajaribu kusaidia ili haki ya watu waliouawa imepatikane.
>
> *Tunu: Na wala si kuwaua watu kama kuku na kuchekacheka kama ... (uk 44)*

Hili ni dondoo ambalo ni maneno ya Tunu kwa Majoka kuashiria kuwa majoka anawaua watu bila kujali. Kulingana na Hashima damu nyingi imemwagika Sagamoyo na imesababisha ardhi kuingia najisi. Hali ambayo imesababisha maziwa na mito kukauka.

Kuna pia mauji na maumivu ambayo yamesababishwa na matumizi ya pombe haramu na dawa za kulevya.

> *Tunu: Haya ndiyo maisha mnayoyataka kuishi kweli? Juzi tuliwazika wangapi kutokana na pombe hii? Wengine wamegeuka vipofu. (Uk 63)*

Hii ni hali ambayo wananchi wameingizwa na viongozi wao kwa sababu pombe hii inanunuliwa na watu wa viongozi hawa. Hii ni kuwakengeusha wananchi wasione mabaya yanayoendelezwa na viongozi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

Majoka na Kenga wanapanga mauji ya Chopi. Mauaji haya yanapangwa kwa sababu Chopi hakupanga mauaji ya Tunu jinsi ilivyokuwa imepangwa. Kwa sasa imejulika na viongozi wa tabaka la juu kuwa amejua mengi na anaweza kutoa siri baada ya kuhojiwa.

> *Majoka : Chopi ni hatari kwetu sasa. Anajua mengi sasa kuliko anavyostahili. Wanaweza kumdadisi na akaropoka.*
>
> *Kenga: Nafikiri Chopi lazima aende safari.*
>
> *Majoka: Naam, na tafadhali iwe one tourch na lisitendeke kosa lolote. Hatuwezi kuifungulia kashfa nyingine mlango. Hiyo ya Tunu najua itatutoa jasho. (Uk 69)*

Mazungumzo baina ya Kenga na Majoka yanaonyesha mpango uliopo wa kumteketeza Chopi ambaye ni mkuu wa polisi. Mpango huu unapangwa kimafumbo kuwa lazima aende safari. Safari hii ni kifo.

Ngurumo anauawa kwa kunyongwa na chatu akitoka Mangwe ulevini. Huu ni mpango ambao umefanywa na Majoka na wafuasi wake kwa sababu Ngurumo alitumwa kumuua Tunu lakini hakumuua bali aliuvunja tu mguu wake. Ili kuficha hii siri ililazimika kuwa Ngurumo ambaye alikuwa na siri hiyo auawe.

> *Chopi: (Anathema.) Mzee nina habari mbaya … za huzuni … ku… kuhusu mtu wetu, Ngurumo …*
>
> *Majoka: Ana nini tena?*
>
> *Chopi: Amenyongwa na chatu akitoka Mangweni*. (Uk 69)

Ngurumo amekuwa mfuasi wa Majoka na Husda. Uhusiano huu ulisababisha yeye na mkewe Asia kupewa kandarasi ya kuoka keki ya uhuru. Uhusiano huu umetoweka kwa sababu ya Ngurumo kutofuata maagizo ya kumuua Tunu. Majoka amewaua watu wengi na kuwarusha katika kimbi. Mwili wa Ngurumo pia utafukiwa juu ya mili mingine. Majoka akiwa amezirai, anaona ziwa kubwa la damu ya watu ambao amekuwa akiua. Anasikia vilio vya watu wakilia kwa uchungu kwa sababu ya vifo alivyosababisha yeye mwenyewe. Anasikia sauti ya Jabali ambaye aliua ikimkaba kooni. Damu ya Jabali pia inatiririka mikononi mwa Majoka.

**Ukosefu wa Chakula**

Haji, (2018) anadai kuwa utabaka na ukengeushi husababisha hali ya umasikini kwa sababu watu hutumia muda mwingi kupigana badala ya kushughulikia masuala ya maendeleo. Katika tamthilia ya *Kigogo*, utabaka na ukengeushi umesababisha hali ya kupanda kwa bei ya chakula. Wananchi masikini kama vile sudi wanakosa chakula cha kuwalisha watoto wao.

> *Pili: (Anaondoka ndani ya nyumba ghafla.) Shikamoo baba! ( Kwa Sudi huku akitokwa na machozi.) Nataka chakula. Nina njaa … (uk 17)*

Pili ni mtoto wa Sudi na Ashua. Kwa sababu ya umasikini, hawana chakula cha kumpa huyu mtoto. Kwa wakati huu, Ashua ameenda kwa Majoka kuomba chakula.

> *Ashua: (Kwa mnong'ono.) Wanangu wamelala njaa … hawajala.*
>
> *Majoka: (Kwa mnong'ono.) Usijali Ashua. Haja zako ni haja zangu, shida zako ni shida zangu, na kiu yangu ni kiu yako. Bora maelewano tu. (Anataka kupiga busu. Ashua anajifuruta na kuruka kando, karibu na mlango.) Warukaje kama kiroboto? Hivyo ndivyo unavyosema na umpendaye? (uk 22-23)*

Kwa sababu ya ukosefu wa vyakula, Ashua anamwambia Sudi kuwa hawezi kuwalisha watoto wake. Mazao pia ni machache ambayo hayawezi kutoa chakula cha kutosha msimu mzima. Hali hii imesababishwa na soko kufungwa na biashara kukosa kuendelea. Mazungumzo ya Siti na mamake

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

yanaashiria kuwa mchele hautatosha kukimu mahitaji ya jamii.

*Siti: Naona mmevuna vizuri msimu huu.*

*Hashima: Wapi? Kichele hiki tu, hata hakipikiki mkate wa sinia. Sijui tutakula nini tukingoja soko kufunguliwa. (uk 52)*

Hii ni hali mbaya ya uchumi kwa Wanasagamoyo kwa sababu soko limefungwa na hawawezi kufanya biashara. Kwa wakati huo, chakula pia hakipo. Hali hii imesababishwa na serikali ya Majoka ili watu wa tabaka la chini wasiwe na nguvu ya kupinga uongozi wake mbaya.

**Watu kufukuzwa Kwao**

Watu wanabaguana kwa misingi ya ukoo wao. Wanajamii ambao asili yao ni kwingine wanatimuliwa ili warudi kule walikozaliwa. Chuki hii huchochewa na viongozi ambao wanataka wabaki mamlakani na kuendelea kuwa katika tabaka la juu. Viongozi huwakengeusha wananchi wa kabila lao ili kuwatumia kuwatimua wengine katika eneo fulani. Ndemo, (2014) anadai kuwa Wakenya walipigana kwa misingi ya kikabila iliyosababisha matabaka ya masikini na matajiri. Kila kabila lilijiona kuwa bora na hilo ndilo lilitaka kuwa uongozini. Katika Tamthilia ya Kigogo, hali hii inasababisha vijikatarasi vya vitisho kurushiwa akina Siti kuwa wahame mahali ambapo wanaishi kwa sasa. Katika vijikaratasi hivyo, Siti wanaambiwa wahame pale Sagamoyo kwa sababu Sagamoyo si kwao. Wanatishiwa kuwa watakomeshwa kama siafu. Hii inamaanisha kuwa watafukuzwa kwa nguvu kutoka pale wanapoishi.

*Siti: Pole mama, hata sisi ni hivyo hivyo. Jana walitutupia vijikaratasi.*

*Hashima: Vya nini tena?*

*Siti: Vitisho, wajua tangu jirani yetu Sudi aingilie siasa alituchongea.*

*Hashima: Najua mwanangu, nayaelewa yote. Twaishi kwa neema. Vijibarua vyenyewe vyasema nini?*

*Siti: Tuhame Sagamoyo. Sagamoyo si kwetu.* (Uk 51-52)

Hali hii inaashiria kuwa kuna watu ambao hawatakikani kuwa Sagamoyo kwa madai kuwa Sagamoyo si kwao. Hii hii inaweza kuzua vita vya kikabikabila kwa sababu kuna wale wanaoona kuwa wananyanyaswa. Kuna wale wanaoona kuwa wanaishi na maadui.

**Mapinduzi**

Mapinduzi hutokea wakati wananchi wamechoshwa na uongozi mbaya. Wananchi humuondoa kiongozi dhalimu na kumchagua kiongozi ambaye wana imani naye kuwa atawaongoza kwa njia iliyo nzuri. Mapinduzi yanatokea katika nchi ya Sagamoyo na kumtimua Majoka mamlakani. Hali hii ni sawa na utafiti wa (Ali 2015) ulioonyesha kuwa kuna wahusika wa kimapinduzi katika riwaya ya *Zawadi ya Ushindi* (Ali, 2015). Majoka anaondolewa mamlakani kwa nguvu. Katika lango kuu la soko la Chapakazi, watu wanamzomea Majoka kwa kuwaita wajinga. Tunu anapewa kinasasauti kutoka kwa mwanahabari, Tunu anawahutubia wananchi huku watu wakimshangilia. Anawaambia watu kuwa hawatoki hapo kabla soko halijafunguliwa. Mkuu wa polisi pia amejiunga na kikundi cha Tunu kwa kuwapa usalama badala ya kuwatawanya wananchi jinsi walivyofanya awali.

Wananchi wanakubaliana kuwa hawawezi kuwachagua viongozi ambao watawaita wajinga. Kingi anakiuka amri ya kutowapiga wananchi risasi kwa sababu wanalindwa na katiba. Kwa mara ya kwanza, katiba inatumiwa kuwalinda wananchi wa tabaka la chini. Kingi anamweleza Majoka kuwa katiba ina mamlaka makubwa kuliko amri ya kiongozi kama vile Majoka. Katiba pia inailinda kazi ya Kingi kama mkuu wa polisi na Majoka hana

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

mamlaka ya kufuta kazi bila kufuata mchakato uliowekwa na katiba.

Kenga ambaye amekuwa mfuasi mkubwa wa Majoka anaondoka upande wa Majoka na kujiunga na kikundi ambacho kimekuwa pinzani cha Tunu. Kingi pia anajiunga na wapinzani, jambo ambalo linasababisha walinzi pia kuwacha kumlinda Majoka na kujiunga na kikundi cha Tunu. Kwa wakati huu Majoka hana mamlaka juu ya watu kwa sababu hana ulinzi wa askari. Kwa hivyo, anajitia ukakamavu wa bandia. Wananchi wanafungua soko la Chapakazi wakiongozwa na Tunu. Mamapima pia anaungama mabaya ambayo aliwafanyia wanasagamoyo. Anajiunga na Kikundi cha Tunu kwa sababu pombe yake imemwagwa. Anakaribishwa na Tunu kwa sababu Tunu amekuwa akipigania usalama wa Wanasagamoyo wote. Sudi anakiri kuwa sasa kuna uhuru katika nchi ya Sagamoyo. Tunu anatunukiwa kuwa shujaa wa Sagamoyo.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Makala haya yalilishughulikia athari za utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya Kigogo iliyoandikwa na Pauline keya. Ilibainika kuwa utabaka na ukengeushi husababisha kuteseka kwa wananchi wa tabaka la chini huku viongozi katika tabaka la juu wanajilimbikizia mali. Hali hii imesababishwa na ufisadi ambapo mali ya wananchi wa Sagamoyo inatumiwa kwa mahitaji ya kibinafsi. Majoka anafunga soko la Chapakazi kwa nia ya kulinyakua shamba hilo ili ajenge hoteli ya kifahari ambayo ingekuwa ya kibinafsi. Hii ingemnufaisha yeye na familia yake pekee. Majoka ameanzisha biashara ya ukataji miti katika nchi ya Sagamoyo bila kujali kuwa hali hio inasababisha uchafuzi wa mazingira. Uchafuzi mwingine wa mazingira unajitokeza wakati soko la Chapakazi halisafishwi ilhali wafanyibiashara wanalipa kodi. Kulingana na Ashua, wafanyikazi hawalipi kodi tu bali kodi na kitu kingine juu yake ilhali soko halisafishwi. Hali hii inasababisha ukosefu wa maendeleo kwa sababu wananchi wanahisi kuwa mahitaji yao hayashughulikiwi. Chakula kinakosekana na kile ambacho kipo kinauzwa kwa bei ghali ambayo haiwezi kufikiwa na wananchi wa kawaida kama vile Ashua, Boza na Sudi.

Kuna mauji ya wapinzani wa Majoka kama vile Jabali ambaye alikuwa mpinzani wa Majoka katika kipindi cha uchaguzi uliopita. Kifo chake kinapangwa na Kenga kwa kutumia ajali ya barabarani. Mpango huu unafanywa ili Majoka aendelee kuwa kiongozi ingawa hapendwi na wananchi. Kwa sababu ya hali ya umasikini, Majoka anachukulia hali hii na kuendeleza usherati wake kwa wa watu walio masikini. Anamtaka Ashua kimapenzi ndipo ampe msaada wa chakula. Kwa hivyo jamii ya Sagamoyo ni jamii ambayo masikini anastahili kuwa masikini lakini matajiri wanatumia mbinu zote ili kubaki kuwa katika tabaka la juu. Ndio maana wananchi wa tabaka la chini wanaungana na kupindua serikali ya Majoka na kufanya Tunu kuwa kiongozi wao mpya. Hii ni hali inayooana na nadharia ya umarks ambayo inapendekeza kuwepo kwa mapinduzi katika utawala unaowanyanyasa wanyonge.

### Mapendekezo kwa Tafiti Zingine

Makala yalishughulikia athari za utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya Kigogo. Kwa hivyo, makala haya yanapendekeza utafiti mwingine ufanywe kuhusu athari za utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya *Kilio cha Haki*. Makala haya pia yanapendekeza utafiti mwingine ufanywe kuhusu athari za utabaka na ukengeushi katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Nguu za jadi*.

## MAREJELEO

Abdille na Wenzake, (2017), Usasabaadaye Katika Riwaya ya Walenisi, *Sumait University Journal.Victoria 3053.*

Castle, G. (2007), *The Blackwell Guide to Literary Theory*, Victoria, Blackwell Publishing

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2645

Gakii, I. (2019), *Mwingiliano Matini katika tamthlia za Kifo Kisimani na Fumo Liyongo*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kinoti, T. (2019), Umbuji wa Wahusika katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka kwa Diwani ya Jicho la Ndani (S.A. Mohamed, 2002). *East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature, ISSN 2617-443X | ISSN 2617-7250.*

Mhando R. (2015*) Kuchunguza Dhamira za Kijamii Katika Tamthiliya ya Kiswahili: Mfano wa Tamthiliya ya Hatia ya Penina Mlama*, Tasnifu ya Uzamilia Ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Habib, M. (2005), *A History of Literary Criticism*, Victoria 3053, Blackwell Publishing.

Haji (2018), *Uhalisia wa Utabaka Katika Tamthili ya za Janga la Werevu na Kitumbua Kimeingia Mchanga*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

Masinde, D. (2016), Uhasi Wazi wa Maudhui Katika Tamthilia Teule za Kiswahili Nchini Kenya.*Journal of Education and Practice. ISSN 2222-1735 Vol.7.*

Musyoki. C. (2016), *Maudhui ya Ubaguzi Katika Mhanga Nafsi Yangu.* Tasnifu ya Uzamili Ya Chuo Kikuu Cha Nairobi.

WanyonyinaNyandiba, (2016), Uhasi Wazi wa Maudhui Katika Tamthilia Teule za Kiswahili Nchini Kenya. *Journal of Education and Practice ISSN 2222-288X (Online) Vol.7, No.14*.

Tendwa A. (2017), *Kuchunguza Mchomozo Katika Fasihi ya Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Ushairi Katika Diwani ya Ustadhi Andanenga*, Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzani.

Mayieka, M. (2015), *Masuala Ibuka katika Riwaya za Kisasa: Kidagaa Kimemwozea na Mhanga Nafsi Yangu*, Tasnifu ya Uzamili Katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwenda, N. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Augustana College, Rock Island, IL 61201

Nayar K. (2010), *Contemporary Literary and Cultural theory*. Delhi, Longman.

Ndemo, (2014), *Uchanganuzi wa Lugha ya Amani na Maridhiano Katika Muziki Nchini Kenya (2008 -2012*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Moi.